**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

*Tele: +255 0262322761-5*
*Fax No. +2550262324218*
**Email:**info@bunge.go.tz

Ofisiya Bunge
S.L.P 941
**DODOMA**

## TAARIFA KWA UMMA

Mheshimiwa Job Ndugai (Mb) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameielekeza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kukutana ili kuchunguza na kujadili kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka, inayodhalilisha Bunge.

Mheshimiwa Spika amechukua hatua hiyo kufuatia kauli zilizonukuliwa katika mitandao ya kijamii kwa lugha za kimasai, kiswahili na kiingereza, zikiashiria kejeli na dharau kwa Bunge na hivyo ameelekeza kuwa wakati wa kuchunguza suala hilo Kamati imuite na kumuhoji ili kubaini ukweli na dhamira ya kauli hizo na kutoa mapendekezo kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwa na Bunge.

**Imetolewa na:** Ofisi ya Spika
S.L.P. 941
**DODOMA**

09 Januari 2018